# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA TISA

**08 SEPTEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 08 SEPTEMBA, 2023

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWAASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kwa Kipindi cha tarehe 01 Julai, 2021 hadi 30 Juni, 2022.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**122. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatambua utaratibu wa Mgodi wa GGML wa ku-*blacklist* Vijana nchini na ni Vijana wangapi wapo *blacklisted*.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**123. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi wa kutosha Wilayani Ludewa hususan katika eneo la Elimu, Afya na Uvuvi.

**124. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza Posho za Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**125. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**126. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya bei ya nauli za Shirika la Ndege Tanzania.

**127. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Madarasa na Mabweni ya Chuo cha Usafirishaji - Mabibo.

**WIZARA YA FEDHA:**

**128. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kwa nini Kodi ya Mapato kwa Wachimbaji wadogo wa madini isiunganishwe na *Mineral Market Management Information System*.

**129. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini mpango wa Serikali katika kunusuru uchumi wa nchi kutokana na ukosefu wa fedha za Kigeni hususani Dola za Kimarekani.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**130. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini huduma ya Mawasiliano ya Simu itapelekwa Kata za Bwawani, Oldonyowas, Laroi, Mwandet, Oljoro na Oldonyosambu.

## WIZARA YA UJENZI:

**131. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Njia Panda - Mangola - Matala hadi Lalago kwa kiwango cha lami.

**132. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini barabara ya Ulinzi ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere inayojengwa toka Liwale hadi Mahenge itakamilika.

**133. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ipo tayari Kujenga Kivuko cha Juu Barabara ya Njia Nane eneo la Magari Saba Mbezi ili kulinda uhai wa Wananchi.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**134. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaviendeleza Viwanda vya Nyama na Samaki Mkoani Rukwa.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**135. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, mchakato wa ujenzi wa Geti jipya la kuingilia Hifadhi ya Mikumi kutokea Kilangali na Tindiga umefikia hatua gani.

## WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

**136. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, lini Serikali itafungua Ofisi za Balozi katika nchi za Iran na Pakistan.

**WIZARA YA AFYA:**

**137. MHESHIMIWA ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA (MTONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa Bima ya Afya kwa Watoto wasio na Wazazi ambao walikuwa wakilipiwa Bima na Wahisani.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**138. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaunga mkono juhudi za Wananchi kwa kumalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Itumbi na Kambikatoto – Lupa.

**139. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itamaliza kazi ya kuwapatia Wananchi Vitambulisho vya Taifa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**140. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itafanya marekebisho ya Sheria zisizo rafiki kwa Wavuvi nchini.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023].*

## V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

**WAZIRI MKUU:**

## VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **08 SEPTEMBA, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |